
# Bwana ni karibu


Zaburi 144,23,89,1718

Siku ya Mungu ya 25 Mwaka A

Rodriguez NTUGULO



1.Kila siku nataka kukusifu, ee Bwana,
na kutukuza jina lako daima na milele.
Bwana ni mkubwa, wakusifiwa sana,
wala ukubwa wake hauvumbulikani.

2. Bwana ndiye mwenye huruma na mpole,
mvumilivu na mwingi wa wema.
Bwana ni mwema kwa wote,
na huruma yake juu ya kazi zake zote.

3. Bwana ni mwenye haki katika njia zake zote,
na mwema katika kazi zake zote.
Bwana ni karibu na wote wanaomwita,
wote wanaomwita kwa uaminifu.